VICTORY HEALTH AND ALLIED SCIENCES COLLEGE
P. O. Box 121 – TABORA
NACTE REG/HAS/209
Phone: +255 (0) 626579274
+255 (0) 622615292
Web: www.vihasco.ac.tz
E-mail: vihasco@yahoo.com
Advance your carrier, enhance learning

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KOZI YA STASHAHADA (DIPLOMA) YA FAMASI MWAKA WA MASOMO 2024/2025

Ndugu, ……..

Ninayo furaha kukujulisha kuwa, umechaguliwa kujiunga na Victory Health and Allied Scieces College (VIHASCO) kusoma kozi ya Famasi ngazi ya Diploma.

Chuo kipo mkoa wa Geita, Ushirombo mjini eneo la Inala km 20 kutoka Tabora mjini barabara iendayo Dar es Salaam.

1. MUDAWA KUFUNGUACHUO

Chuo kitafunguliwa tarehe 02/09/2024, hivyo utatakiwa kufika chuoni kuanzia tarehe hiyo Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/9/2024. Kutakuwa na programu ya mafunzo ya komputa na kingereza cha taaluma ya Famasi yatakayotolewa bure. Programu hii itaanza tar. 5/9/2024 hadi tar 5/10/2024

2. MAELELEZO YA JUMLA WAKATI UNAFIKA CHUONI

(i) Ada inapolipwa haitarudishwa ama kuwekwa kwaajili ya mwaka mwingine wa masomo, au kuwekwa kwa ajili ya matumizi mengine hivyo fanya maamuzi sahihi ya kulipa ada kwa ajili ya masomo;
(ii) Hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kuingia darasani bila kufanya malipo ya ada pamoja na michango ya awamu ya kwanza kama ilivyoelekezwa au kuonyesha katika jedwali hapo chini;
(iii) Pesa ya mitihani italipwa kila mwaka na kiasi kilichoonyeshwa kweny jedwaali lililoko hapo chini ni kwa ajili ya mwaka wa masomo 2024/2025 tu kwa sababu kiwango hicho kinaweza kubadilika wakati wowote kutokana na maagizo ya serikali au kupanda kwa gharama za maisha.

3. SHERIA ZA CHUO , TARATIBU ZACHUO NA SERA ZA MITIHANI

Kila mwanafunzi atapatiwa nakala ya sheria, taratibu na sera za chuo siku chache baada ya kufika chuoni. Kila mwanafunzi atatakiwa kuzisoma sheria na taratibu hizo ili kupata maelekezo na miongozo ya kipindi chota mwanafunzi atakapokuwa Chuoni.

Yafuatayo ni baadhi ya makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa Chuoni.

(i) Wizi, Uasherati na matumizi ya madawa ya kulevya;
(ii) Kuharibu mali za chuo kwa makusudi au kwa uzembe;
(iii) Ugomvi;
(iv) Kushindwa masomo (Kutofikia wastani wa ufaulu katika masomo kulingana na miongozo);
(v) Utoro wa bila taarifa na
(vi) Migomo

4. USAJILI

Mara tu baada ya kufika Chuoni utatakiwa kufika ofisi ya Udahili ili kukamilisha usajili na uwekaji wa kumbukumbu zako. Endapo utafika Chuoni baada ya muda wa kazi (Saa 10.00) au siku za sikuku, Juma Mosi na Juma Pili, tafadhali piga simu namba **062 6579274** uweze kupatiwa msaada wa kupokelewa.

Ukifika Chuoni utatakiwa kuwaslisha vitu vifuatavyo kwa matumizzi ya ofisi:

(i) Vivuli vya vyeti sawa na idadi uliyofanya mitihani ya kidato cha nne au cha sita;
(ii) Picha nne (4) (passport size);
(iii) Risiti za benki zinazothibitisha malipo ya ada na michango uliyolipa;
(iv) Fomu ya maelezo ya kujiunga (Joining Instructions);
(v) Wanafunzi wanaotoka nje ya Tanzania wanatakiwa kuwasilisha hati ya kusafiria (passport);
(vi) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa;
(vii) Fomu iliyojazwa ya kupimwa afya (Medical examination) iliyothibitishwa na Daktari kutoka kituo chochote cha afya kinachotambuliwa na serikali (fomu imeambatanishwa)
(viii) Fomu ya kiapo iliyojazwa kwa taarifa sahihi (Fomu imeambatanishwa)

5. MALAZI

(i) Chuo kinatoa huduma ya kulala wanafunzi wote bila kujali mwanafunzi anatokea wapi isipokuwa kwa wale wenye sababu maalumu za kukaa nje ya bweni za chuo ambazo zimedhibitishwa na mkuu wa chuo. Huduma ya malazi inatolewa bure;
(ii) Mwanafunzi atatakiwa kufika na vitu vifuatavyo kwa ajili ya matumizi yake binafsi na malazi Godoro dogo lenye upana wa futi 3 na urefu wa futi 6; Mashuka mawili (rangiyoyote), blanket, Taulo, Ndala, Neti na Ndoo.

6. SARE ZA CHUO

Wanafunzi wote watatakiwa kuvaa sare za chuo kama zilivyopendekezwa na uongozi wa chuo, Sare kwa wanafunzi wote hutolewa chuoni siku chache baada ya wanafunzi kuripoti.

Sare zinazotolewa ni Gauni 1 nyeupe na koti 1 ya maabala kwa wasichana na Suruali moja ya kaki, shati 1 nyeupe na koti ya maabala kwa wavulana. Mwanafunzi atatakiwa kuja na viatu vya chini vilivyofunikwa vyenye rangi nyeusi na soksi nyeupe. Nguo za nyumbani zinazoendana na maadili ya Kitanzania zinaruhusiwa baada ya muda wa masomo.

7. CHAKULA

Chuo kina mgahawa ambao hutoa huduma ya chakula kwa bei ndogo. Mwanafunzi anaweza kulipia shilingi za Kitanzania 75,000/= kwa mwezi au kwa kununua c h a k u l a k a f t e r i a mwenyewe kila siku. Pesa ya chakula haitalipwa chuoni bali italipwa kwa mzabuni wa chakula.

8. VIFAA VYA DARASANI (STATIONERY)

Kila mwanafunzi atatakiwa kuja na rimu 4 za karatasi zenye ukubwa wa A4. Hii itakuwa ni kila mwaka wa masoma. Mwanafunzi anaweza kuleta rimu mbili(2) anapofika Chuoni na nyingine mbili zitaletwa wakati wa kuanza muhula wa pili. Lakini pia kila mwanafunzi atatakiwa kuja na madaftari angalau 7, kalamu za kutosha, rula, penseli, seti ya mahesabu (mathematical set), taulo ndogo mbili kwa ajili ya maabara, box moja la glovu (Examination gloves) na Scientific mathematical calculator moja.

9. ADA NA MICHANGO MIGINE

Kila mwanafuzi atapaswa kulipa ada ya chuo na michango mingine kwa kufuata mchanganuo ufuatao:

S/N	Aina ya malipo	Jumla ya Pesa itakayolipwa kwa mwaka	Muda wa kulipa	MCHANGANUO WA MUDA WA MALIPO			
				Awamu ya I	Awamu ya II	Awamu ya III	Awamu ya IV
				Unapofika Chuoni	Mwezi Desemba	Mwezi Machi	Mwezi Juni
A	**Ada ya masomo (Tuition fee)**						
1	**Ada ya masomo**	**1,650,000**	Kila mwaka	**450,000**	**400,000**	**400,000**	**400,000**
B	**Michango**						
1	Ada ya usajili wa mwanafunzi	20,000	Unapowasili chuoni	20,000			
2	Ada ya NACTVET ya uthibiti ubora	20,000	Kila mwaka	20,000			
3	Ada ya mitihani ya Wizara ya Afya	150,000	Kila mwaka			150,000	
4	Ada ya mitihani ya ndani	100,000	Kila mwaka	100,000			
5	Ada ya Serikali ya Wanafunzi	5,000	Kila mwaka	5,000			
6	Pesa ya tahadhari	50,000	Unapowasili chuoni	50,000			
7	Pesa ya kununua kitambulisho	10,000	Kila mwaka	10,000			
8	Pesa ya sare ya Chuo	70,000	Unapowasili chuoni	70,000			
9	Pesa ya kununua Tisheti	10,000	Unapowasili chuoni	10,000			
10	Pesa ya kununua vitabu vya mazoezi ya vitendo (TPH)	50,000	Unapowasili chuoni		50,000		
11	Pesa ya kulipia mazoezi ya vitendo (Field)	150,000	Kila mwaka		150,000		
12	Pesa ya kulipia Bima ya afya kwa wasiokuwa na bima	50,400	Kila mwaka	50,400			
13	Pesa ya kununua kitabu cha kuweka kumbukumbu za mafunzo ya vitendo (Procedure books)	20,000	Kila mwaka	20,000			
	Jumla ya Michango			**355,400**	**200,000**	**150,000**	
	Malipo ya Bweni	Bure		Bure	Bure	Bure	Bure
	Jumla kuu	**2,355,400**		**805,400**	**600,000**	**550,000**	**400,000**

Malipo yote yaliyoorodheshwa katika kipengele cha Ada na michango kulingana na awamu yalipwe kabla ya kuripoti chuoni kupitia Benki ya **NMB** akaunti namba **51010074169, J**ina: **Victory health and allied sciences college** Tawi la Tabora

Tunakutakia maandalizi mema ya kujiunga na VIHASCO.

Karibu Victory Health and Allied Sciences College kwa Elimu bora na yenye mafanikio.

Wako

Gift Nnko

MKUU WA CHUO - VIHASCO



FOMU YA KIAPO

Mimi,_____Ninathibitisha kwamba kwa akili yangu timamu nimesoma na kuelewa fomu ya maelezo ya kujiunga na chuo cha Victory Health and Allied Sciences College na ninaahidi kufuata maelekezo kama yalivyoelekezwa.

Sahini……..Tarehe……..

VICTORY HEALTH AND ALLIED SCIENCES COLLEGE
P. O. Box 121 – TABORA
NACTE REG/HAS/209

Advance your carrier, enhance learning

Web: www.vihasco.ac.tz E-mail: vihasco@yahoo.com, phone: +225 626 579 274/ +225 622615292

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

FULL NAME ……..

Please check the above named to his/her physical and mental fitness:

Eyesight…….....

Hearing…….....

Limbs…….....

Speech…….....

Venereal diseases/STD…….....

Leprosy…….....

Epilepsy…….....

Neurosis…….....

Diabetic mellitus.....

Tuberculosis.....

Hemoglobin Level.....

Pregnancy.....

Any other deformity (specify).....

Other seriousdisease (specify).....

He/she is physically fit/unfit to follow this course

Certification:

Name…….Title……

Signature…….....Date……..

Station:……..Stamp.....